

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA NANE  
(DAILY SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS)**

**04 FEBRUARI, 2015**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**  
**YATOKANAYO NA KIKAO CHA NANE**  
**(SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS - EIGHTH SITTING)**  
**TAREHE 4 FEBUARI, 2015**

**I. DUA:**

Dua ilisomwa saa 3.00 asubuhi na Mhe. Mussa Azan Zungu (Mb) na Kikao Kiliendelea.

Makatibu Mezani:

1. Ndg. Justina Shauri
2. Ndg. Neema Msangi
3. Ndg. Joshua Chamwela

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Huduma za Jamii kwa Kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari 2015.

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa Kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari 2015.

**III. MASWALI:**

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa:

**1. OFISI YA WAZIRI MKUU:**

SWALI NA. 83: Mhe. Dkt. David Malole (Mb) (liliulizwa Mhe. H. Chibulunje)

Nyongeza:

- (i) Mhe. Hezekiah Chibulunje, (Mb)
- (ii) Mhe. Mohamed Ali Keissy, (Mb)
- (iii) Mhe. Diana Mkumbo Chilolo, (Mb)

SWALI NA. 84: Mhe. Deogratias Ntukamazina, (Mb)

- Nyongeza: (i) Mhe. Deogratias Ntukamazina, (Mb)  
(ii) Mhe. Pauline Philip Gekul, (Mb)  
(iii) Mhe. Michael Lekule Laizer, (Mb)  
(iv) Mhe. Joseph Roman Selasini, (Mb)

SWALI NA. 85. Mhe. Said Mohammed Mtanda, (Mb)

- Nyongeza: (i) Mhe. Said Mohamed Mtanda, (Mb)  
(ii) Mhe. Idd Mohamed Azzan, (Mb)

## 2. WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

SWALI NA. 86: Mhe. Ritta Enespher Kabati, (Mb)

- Nyongeza: (i) Mhe. Ritta Enespher Kabati, (Mb)  
(ii) Mhe. Hamad Ali Hamad, (Mb)  
(iv) Mhe. Benedict Ole Nangoro, (Mb)

## 3. WIZARA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

SWALI NA. 87: Mhe. Joseph Roman Selasini, (Mb)

- Nyongeza: (i) Mhe. Joseph Roman Selasini, (Mb)

## 4. WIZARA YA UCHUKUZI:

SWALI NA. 88: Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, (Mb)

- Nyongeza: (i) Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, (Mb)  
(ii) Mhe Aliko Nikusuma Kibona, (Mb)

5. WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

SWALI NA. 89: Mhe. Kidawa Hamid Saleh, (Mb)

Nyongeza: (i) Mhe. Kidawa Hamid Saleh, (Mb)  
(ii) Mhe. Martha Moses Mlata, (Mb)  
(iii) Mhe. Zitto Zuberi Kabwe, (Mb)  
(iv) Mhe. Mohammad Ibrahim Sanya, (Mb)

SWALI NA: 90: Mhe. Maryam Kisangi, (Mb) (liliulizwa na Mhe. Ndugulile)

Nyongeza: (i) Mhe. Faustine Ndugulile, (Mb)  
(ii) Mhe. John Momose Cheyo, (Mb)

6. WIZARA YA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO:

SWALI NA: 91: Mhe. Amina Mohammed Mwidau, (Mb)

Nyongeza: (i) Mhe. Mariam Msabaha, (Mb)

7. WIZARA YA FEDHA:

SWALI NA: 92: Mhe. Conchesta Rwamlaza, (Mb)

Nyongeza: (i) Mhe. Conchesta Rwamlaza, (Mb)

8. WIZARA YA KAZI NA AJIRA :

SWALI NA: 93: Mhe. Rajab Mbarouk Mohammed, (Mb)

Nyongeza: (i) Mhe. Rajab Mbarouk Mohammed, (Mb)

9. WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

SWALI NA: 94: Hamoud Abuu Jumaa, (Mb)

Nyongeza: (i) Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, (Mb)

10. WIZARA YA MAMBO YA NDANI:

SWALI NA. 95: Mhe. Shaffi Ahmedali Sumari, (Mb)

Nyongeza: (i) Mhe. Shafin A. Sumar, (Mb)

11. WIZARA YA MAJI:

SWALI NA: 96 Mhe. John Zefania Chiligati, (Mb)

Nyongeza: Mhe. (i) John Zefania Chiligati, (Mb)

SWALI NA: 97: Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, (Mb)

Nyongeza: (i) Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, (Mb)

**III. MATANGAZO:**

(a) Wageni wote waliokuwepo katika gallery ya Spika na gallery ya Maafisa walitambulishwa.

(b) **KAZI:**

Kamati ya Huduma za Jamii ikutane ukumbi na 227 saa 7.00 mchana.

#### **IV. MWONGOZO WA SPIKA:**

- Mhe. Kabwe Zuberi Zitto (Mb) aliomba Mwongozo kupitia Kifungu 68(7) kuhusu maswali ya Wabunge kutokujibiwa kikamilifu kwenye Swali Namba 89 la Mhe. Kidawa Hamid Saleh (Mb), Kwamba Waziri hakujibu kabisa swali hilo pamoja na maswali yake ya nyongeza.
- Mwenyekiti alimuomba Waziri akutane na Mbunge na ampatie majibu sahihi.
- Mhe. Kisyeri Chambiri (Mb) aliomba muongozo kupitia kifungu cha 98(7) kuwa wananchi wa Babati Mjini wamekopwa mazao yao na hawajalipwa hadi leo, je ni lini watalipwa fedha zao.
- Mwenyekiti alitoa uamuzi kuwa Kanuni aliyotumia siyo sahihi ila Waziri akutane nae na ampatie majibu ya maswali aliyouliza.
- Mhe. James Mbatia (Mb) aliomba mwongozo kutumia Kanuni ya 47 kuhusu Bunge kujadili jambo la dharura lenye maslahi kuhusu uandikishaji wa daftari la kudumu la wapiga kura ambalo kwa sasa halipo na linatakiwa kuanzishwa upya, na kufuatia Taarifa kuwa jana Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanzisha suala hilo katika baadhi ya Mikoa hivyo ni vema suala hilo muhimu lijadiliwe na Bunge.
- Mwenyekiti alitoa uamuzi kwa wadau muhimu wa suala hilo ikiwemo Serikali na Kamati ya Uongozi wakae kuliangalia suala hili.

#### **V. HOJA ZA KAMATI:**

- Mhe. John Zefania Chiligati (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama aliwasilisha maoni ya Kamati na kutoa Hoja kuwa Bunge likubali Taarifa ya Kamati pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.
- Mhe. Selemani Said Jafo (Mb), Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa aliwasilisha Taarifa ya Kamati na kutoa Hoja ya kuliomba Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati pamoja na Mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.
- Mhe. Luhanga Joelson Mpina (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara aliwasilisha Taarifa ya Kamati na kutoa Hoja kuwa

Bunge lipokee na kuikubali Taarifa hiyo Pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

**VI. UCHANGIAJI:**

Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kuchangia Hoja za Kamati:-

(1) Mhe. Idd Mohammed Azzan (Mb) – CCM

(2) Mhe. Rosweeter Faustine Kasikila (Mb) – CCM

**VIII. KUSITISHA BUNGE:**

Saa 7.00 mchana Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Lediana Mafuru Mng'ong'o alilisitisha Bunge hadi saa 11.00 jioni.

**IX. BUNGE KUREJEA:** Saa 11.000 jioni Bunge lilirudia likiongozwa na Mwenyekiti Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) na Mjadala wa Hoja za Kamati uliendelea na wafuatao walichangia:-

1. Mhe. Khatib Said Haji (Mb) – CUF
2. Mhe. Naomi Mwakyoma Kaihula (Mb) CHADEMA
3. Mhe. David Zacharia Kafulila (Mb) \_ NCCR – MAGEUZI
4. Mhe. Meshack Jeremiah Opolukwa (Mb) – CHADEMA
5. Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni (Mb) – CCM
6. Mhe. Hamad Rashid Mohammed (Mb) CUF
7. Mhe. Margreth Agnes Mkanga (Mb) – CCM

Baada ya mjadala Mawaziri wafuatao walipewa fursa ya kujibu Hoja zilizotolewa na Wabunge:-

8. Mhe. Christopher Chiza (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji na Uwezeshaji.

9. Mhe. Bernard C. Membe (Mb,) Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

10. Mhe. Saada Salum Mkuya (Mb), Waziri wa Fedha
11. Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (Mb), – Waziri wa Ulinzi na JKT
12. Mhe. Dkt. Abdalaah Omar Kigoda (Mb), Waziri wa Viwanda na Biashara
13. Mhe. Menrard Chikawe (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Wenyeviti wa Kamati tatu zilizotoa Hoja walipata nafasi ya kujibu Hoja za Wabunge kama ifuatavyo:-

- i. Mhe. John Zefania Chiligati (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi alihitimisha Hoja- Bunge lilipitisha Maazimio ya Kamati hii bila ya mabadiliko yoyote.
  - ii. Mhe. Selemani Said Jafo (Mb), Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kamataifa alihitimisha Hoja – Bunge lilipitisha Maazimio ya Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa bila ya mabadiliko yoyote.
  - iii. Mhe. Luhanga Joelson Mpina (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara alihitimisha Hoja .
- Baada ya kutoa Hoja yake, Mwenyekiti wa Bunge alimkaribisha Mhe. Zitto Kabwe atoe Pendekezo lake la kwanza.

#### MAPENDEKEZO YA MHE. ZITTO KABWE

- Mhe. Zitto Kabwe (Mb) alitoa pendekezo lake ambalo liliungwa mkono na Mwenyekiti wa Kamati husika.
- Waziri wa Nchi (Sera Uratibu na Bunge) alitoa maelezo kuwa Serikali iachwe ishughulikie jambo hili kwa wakati mwafaka kwa kuwa muda uliopo ni mdogo sana kuweza kutekelezwa kwa ufanisi na kuja kutoa Taarifa katika Mkutano wa 19.



- Mhe. Mpina (Mb) alisisitiza kuwa muda unatosha Serikali bado inaweza kuja na mkakati kuhusu suala hili.
- Waziri wa Nchi (Sera na Uratibu Bunge) na Waziri wa Viwanda, na Biashara walisitiza kuwa muda uliopo ni mfupi ili kufanya kazi hiyo labda ije Mkutano wa 20.
- Bunge lilikubali Maazimio ya Kamati pamoja na pendekezo la kwanza la Mhe Zitto (Mb) kuwa Taarifa ya Serikali itolewe wakati wa Mkutano wa 20.
- Mhe. Zitto (Mb) alikaribishwa kutoa Pendekezo lake la pili. Ambapo baada ya kulitoa Naibu Waziri wa Fedha, alisema Serikali inakubaliana na pendekezo hilo na itaangalia namna ya kulitekeleza, ila alishauri lugha ya Maazimio itoke na kubaki kama Mapendekezo).

#### MAPENDEKEZO YA MHE. DAVID KAFULILA (Mb)

- Pendekezo la Kwanza- Bunge lilikubali kuwa Serikali ikaangalie uwezekano wa kupunguza riba, na kukataa Maneno Serikali ikapunguze riba .....
- Pendekezo la Pili – Bunge lilipitisha Pendekezo hili kwa kuitaka Serikali ikaifanyie kazi pendekezo hilo.
- Pendekezo la tatu – Serikali iliridhia na Mbunge alitoa pendekezo kwa kuwa limeshachukuliwa na mapendekezo mengine.

**X. KUAHIRISHA BUNGE:**

Saa 2.15 usiku Mhe. Spika aliahirisha Bunge hadi kesho Jumanne tarehe 5/01/2015 saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA  
4 FEBUARI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**